TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tarehe: 14 Aprili 2026

RIPOTI KUU ZA MWAKA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

DODOMA

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha ukaguzi wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25 na kuwasilisha Ripoti Kuu za Mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mnamo tarehe 30 Machi 2026. Kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwenye Katiba, Serikali iliwasilisha Ripoti hizo Bungeni siku ya Ijumaa, tarehe 10 Aprili 2026. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT) inatoa taarifa hii ili kuujulisha umma kuwa ripoti hizo sasa zinapatikana kwa umma kwa ajili ya hatua za kibunge na usimamizi wa wananchi.

Ripoti Kuu za Mwaka zilizowasilishwa

Zifuatazo ni **Ripoti Kuu za Mwaka kwa mwaka wa fedha 2024/25** zilizowasilishwa Bungeni:

- Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Serikali Kuu;
- Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ;
- Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma;
- Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);

- Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi pamoja na ripoti 19 za ukaguzi wa ufanisi katika sekta mbalimbali.

Kwa ujumla, ripoti hizi zinatoa tathmini ya kina ya usimamizi wa rasilimali za umma, mifumo ya utawala, na ufanisi wa utoaji wa huduma katika sekta ya umma.

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi

Jumla ya **kaguzi 1,554** zilifanyika katika mwaka wa fedha 2024/25, zikijumuisha kaguzi za taarifa za fedha 1,339, pamoja na kaguzi za ufanisi, uzingatiaji wa sheria, uchunguzi, ukaguzi unaotumia mbinu ya papo kwa papo (real time), na mifumo. Kati ya kaguzi za taarifa za fedha 1,339 zilizotekelezwa, kaguzi 1,326 sawa na asilimia 99 zilipewa hati safi za ukaguzi.

Wakati akiwasilisha ripoti hizo kwa Rais, CAG alibainisha kuwa kwa ujumla, ripoti za ukaguzi zinaonesha kuwa uandaaji wa hesabu unaridhisha, na kwa kiasi kikubwa, unazingatia taratibu na kanuni za uandaaji wa hesabu hizi. Hata hivyo, CAG alitoa tahadhari kuwa kupata hati safi ya ukaguzi si lazima kuwe na maana kuwa shughuli zote hazina dosari, au kwamba mifumo ya udhibiti wa ndani ni imara kikamilifu, au kwamba wananchi wanapata huduma bora zaidi.

Taasisi zenye Hati zenye Shaka, Hati Mbaya, na Kushindwa Kutoa Maoni

Ingawa asilimia 99 ya taasisi zilifanya vizuri, asilimia 1 iliyosalia inaakisi udhaifu mkubwa. Ni muhimu kwa umma kuelewa maana ya matokeo haya.

- **Hati yenye Shaka:** hutolewa pale ambapo makosa katika taarifa za fedha yana umuhimu wa kifedha lakini hayajaenea kwa kiwango kikubwa, au pale ambapo ushahidi wa kutosha wa ukaguzi haukuweza kupatikana katika maeneo mahsusi. Taasisi zilizopata hati zenye shaka katika mwaka wa fedha husika ni pamoja na Bodi ya Korosho Tanzania, Kiwanda cha Dawa cha Keko, Bodi ya Chai Tanzania, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kondoa, Jumuiya ya Maji Ngazi ya Jamii Kilumsa, Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, pamoja na vyama vya siasa vikiwemo Civic United Front (CUF) na National Reconstruction Alliance (NRA).

- **Hati Mbaya:** hutolewa pale ambapo makosa katika taarifa za fedha yana umuhimu wa kifedha na yameenea kwa kiwango kikubwa, hali inayofanya taarifa hizo za fedha kutokuwa za kuaminika. Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilipata hati mbaya mwaka huu.

- **Kushindwa Kutoa Maoni:** hutolewa pale ambapo ushahidi wa kutosha na unaofaa wa ukaguzi haukuweza kupatikana, na athari zinazoweza kujitokeza zina umuhimu wa kifedha na zimeenea kwa kiwango kikubwa. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela–Kasumulu na Jumuiya ya Maji ya Mambawasa walipata hati ya kushindwa kutoa maoni mwaka huu.

CAG alisisitiza kuwa ukaguzi ni mchakato endelevu ambapo wakaguliwa hushirikishwa muda wote. Hii inaweza kujumuisha kupitia matukio ya kabla na baada ya utoaji taarifa katika miradi ya muda mrefu, ili kuhakikisha matokeo yote yanategemea ushahidi wa kutosha na unaofaa.

Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita

Katika ripoti hizo, CAG ameelezea shaka yake kuhusu mapendekezo ya muda mrefu yaliyodumu kwa kipindi cha miaka 7 hadi 20 bila kutekelezwa, jambo ambalo linaonesha changamoto endelevu katika ufuatiliaji wa utekelezaji na kushindwa kutatua vyanzo vya matatizo. Ripoti hizo pia zinaonesha kuwa ni 36.7% tu ya mapendekezo 38,181 yaliyotolewa katika miaka iliyopita ndiyo yametekelezwa kikamilifu. Hali hii inaakisi utamaduni wa kuchelewesha uwajibikaji, ambao unaendelea kuweka rasilimali za umma hatarini.

Udhaifu huu wa kimfumo katika kusimamia uwajibikaji na kutatua vyanzo vya matatizo siyo dhana tu; unajidhihirisha wazi katika sekta muhimu, kama inavyothibitishwa na muhtasari wa matokeo mtambuka na muhimu ya ukaguzi yaliyowasilishwa hapa chini:

- Katika **sekta ya afya**, udhaifu ulibainika katika ununuzi, uhifadhi, na usambazaji wa dawa na vifaa tiba, ikiwa ni pamoja na dawa zilizokwisha muda wake, uwasilishaji wa dawa zenye muda mfupi wa matumizi, na vifaa ambavyo havitumiki ipasavyo kutokana na mapungufu ya mipango na mnyororo wa usambazaji.

- Katika **sekta ya elimu**, changamoto ni pamoja na miundombinu duni, uhaba wa vifaa vya kujifunzia, usimamizi dhaifu wa udhibiti, na ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi ya elimu, jambo linaloathiri upatikanaji na ubora wa huduma za elimu.

- Katika **sekta ya maji**, kiwango cha maji yasiyozalisha mapato bado kipo juu kwa wastani wa 35%, kikichangiwa na miundombinu iliyochakaa, uvujaji, maunganisho haramu, na mifumo dhaifu ya ufuatiliaji, jambo linaloathiri uendelevu wa kifedha na utoaji wa huduma.

- Katika **sekta ya nishati**, changamoto ni pamoja na ucheleweshaji wa miradi, ongezeko la gharama, usimamizi dhaifu wa mikataba, na kuongezeka kwa viwango vya madeni, vinavyoathiri ufanisi wa kiutendaji na utulivu wa kifedha.

- Katika **maendeleo ya miundombinu na Matokeo ya Ukaguzi wa Kiufundi**, ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya miundombinu ya viwanja vya michezo ulibaini udhaifu mkubwa katika ununuzi, majadiliano ya mikataba, na uthibitishaji wa kazi. Matumizi ya mbinu za ununuzi zisizo na ushindani bila uhalali wa kutosha yalipunguza uwazi na thamani ya fedha. Aidha, mapungufu katika mchakato wa majadiliano yalisababisha mabadiliko yasiyo na msingi katika wigo wa kazi na kujumuishwa kwa gharama zisizostahili. Mapungufu haya yanaonesha kutofuata matakwa ya ununuzi na yanadhoofisha ufanisi, uchumi, na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

Kwa upana zaidi, maendeleo ya miundombinu ikijumuisha barabara yanaendelea kukabiliwa na changamoto za mara kwa mara, kama vile kuchelewa kukamilika kwa miradi, kazi duni, na kupanda kwa gharama. Ukaguzi pia ulibaini matukio ya malipo yaliyofanywa kwa kazi zisizokamilika au zilizo chini ya viwango, yakichangiwa zaidi na usimamizi dhaifu wa mikataba na uangalizi usiotosheleza. Sababu kuu inayochangia ni kucheleweshwa au malipo yasiyotosheleza kwa wakandarasi, jambo ambalo husababisha ucheleweshaji wa miradi na migogoro ya kimkataba.

Usimamizi wa fedha na changamoto za utawala

CAG aliripoti udhaifu unaoendelea ikiwemo:

- Kutofuata sheria na taratibu za ununuzi

- Usimamizi na utekelezaji dhaifu wa mikataba

- Mifumo isiyofaa ya udhibiti wa ndani

- Mikusanyiko dhaifu ya mapato na usimamizi wa madai

- Kuendelea kutegemea ruzuku za serikali kwa baadhi ya mashirika yanayomilikiwa na Serikali

Katika **Mamlaka za Serikali za Mitaa**, changamoto ni pamoja na mapato ambayo hayajawekwa benki, udhaifu katika usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji, usimamizi mbaya wa mawakala wa mapato, na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Katika **sekta ya benki**, matokeo ya ukaguzi yanaonesha changamoto katika usimamizi wa mikopo, utulivu wa kifedha, na usimamizi wa taasisi za kifedha. Hizi ni pamoja na mazoea yasiyo ya kawaida ya ukopeshaji kama vile mikopo inayozidi viwango vya kisheria, dhamana zisizotosheleza au kukosekana kwa dhamana, na matumizi mabaya ya fedha za mkopo. Aidha, kuna matukio ambapo mikopo iliyochelewa sana inaendelea kuainishwa kama inayofanya vizuri, hali inayoonesha udhaifu katika mifumo ya tathmini na ufuatiliaji wa mikopo. Zaidi ya hayo, baadhi ya benki zinakabiliwa na uhaba wa mtaji, vikwazo vya ukwasi, na kuongezeka kwa viwango vya mikopo isiyolipika, ambayo inaleta shaka kama Benki hizo zina uwezo wa kifedha wa kuendelea katika shughuli zake na kusaidia maendeleo ya kiuchumi.

Mifumo ya TEHAMA na ufanisi katika sekta ya umma

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mifumo ya TEHAMA katika sekta ya umma, ikiwa ni pamoja na muunganiko mdogo kati ya mifumo muhimu ya serikali, uwepo wa mifumo inayofanya kazi zinazofanana, na kuendelea kufanya shughuli za kiutendaji nje ya mifumo. Aidha, yalionekana matukio ambapo taasisi hazikutumia mfumo mkuu wa usimamizi wa fedha wa Serikali (MUSE) bila kupata vibali vinavyohitajika. Mazoea haya yanadhoofisha usanifishaji wa mifumo na uzingatiaji wa mifumo iliyowekwa ya usimamizi wa fedha. Kwa ujumla, changamoto hizi zinapunguza ufanisi wa utendaji kazi, zinaathiri kuaminika kwa takwimu, na kudhoofisha uwajibikaji katika utoaji wa huduma.

Maeneo Mapya ya Mapato: Biashara ya Kaboni (Carbon Credits)

Katika maeneo mapya ya mapato, hasa masoko ya kaboni, ukaguzi ulibaini kuwa ingawa Tanzania ina uwezo mkubwa unaotokana na rasilimali zake za misitu na mikoko, fursa hii bado haijatumiwa kwa ufanisi. Miradi mingi ya kaboni haijaanza kufanya kazi, na hakuna mapato ya maana yaliyopatikana licha ya uwepo wa rasilimali hizi. Udhaifu pia ulionekana katika mipangilio ya mikataba kati ya Serikali na waendelezaji binafsi, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa ukomo maalum wa muda, viashiria vya utendaji, na miundo ya malipo. Zaidi ya hayo, kuna mapengo katika mifumo ya ufuatiliaji na uhakiki, huku Serikali ikitegemea zaidi ripoti kutoka kwa waendelezaji bila kuwa na mfumo huru wa uhakiki. Kwa ujumla, mapungufu haya yanapunguza uwezo wa Serikali kufaidika kikamilifu na masoko ya kaboni, kupunguza uwazi katika biashara ya kaboni, na kuathiri uendelevu wa usimamizi wa rasilimali za mazingira.

Uwekezaji wa umma na thamani ya fedha

Licha ya uwekezaji mkubwa wa umma katika sekta muhimu, matarajio yaliyokusudiwa hayafikiwi kila wakati kutokana na mapungufu katika mifumo ya kupanga, kufuatilia, na kutathmini. Katika baadhi ya matukio, miradi iliyokamilika haitumiki ipasavyo, na hivyo kupunguza thamani ya fedha.

Muhtasari wa Ukaguzi wa Ufanisi

Kati ya ripoti 19 za ukaguzi wa ufanisi zilizotolewa, matokeo muhimu yanaonesha kuwa:

- Upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi wasiojiweza bado umejikita katika maeneo ya mijini, na kupunguza upatikanaji kwa wakazi wa vijijini. Aidha, huduma za matunzo kwa wazee bado zina ukosefu mkubwa wa rasilimali, zikiwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi na vituo, jambo linaloathiri ubora wa huduma zinazotolewa.

- Katika eneo la usalama wa chakula, udhaifu ulibainika katika usimamizi wa hifadhi ya nafaka, ikijumuisha viwango visivyotosheleza vya akiba, matatizo ya ubora wa hifadhi, na uratibu mbaya katika ununuzi. Mapungufu haya yanaweka hatari kwenye utulivu wa bei na upatikanaji wa chakula.

- Aidha, changamoto zilibainika katika afya na usalama mahali pa kazi, ikiwa ni pamoja na kuchelewa kushughulikia madai ya fidia ya wafanyakazi, jambo ambalo linaathiri wafanyakazi wanaopata ajali au madhara kazini.

Maendeleo chanya

CAG alibainisha maendeleo chanya, ikiwemo:

- Kuboreka kwa utoaji wa taarifa za kifedha katika taasisi za umma

- Kiwango kikubwa cha hati safi za ukaguzi (99%)

- Utendaji mzuri katika makusanyo ya mapato ya ndani yakizidi 99% ya malengo

Maboresho haya yanatoa msingi wa kuendelea kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Muhtasari wa Mapendekezo

Kulingana na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi, ripoti inatoa mapendekezo kadhaa kwa ajili ya maboresho. Ufuatao ni Muhtasari wa mapendekezo makuu ya ukaguzi :

- Kuimarisha usimamizi wa miradi na mikataba ya umma ili kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa wakati, inakidhi viwango vya ubora vinavyohitajika, na inakamilika ndani ya gharama zilizodhibitiwa, ili kuepusha hasara na matumizi yasiyo na ufanisi ya fedha za umma.

- Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji na udhibiti wa ndani, hususan katika utoaji wa taarifa za kifedha, usimamizi wa rasilimali, na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

- Kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na usimamizi wa madai kwa kuimarisha ufuatiliaji wa wadaiwa na kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinatimiza wajibu wao wa kulipa ankara kwa wakati.

- Kuimarisha ufanisi wa taasisi za umma na mashirika ya kibiashara kwa kuhakikisha kuwa uwekezaji unaleta tija, kupunguza utegemezi wa ruzuku, na kuboresha usimamizi wa gharama za uendeshaji.

- Kuimarisha usimamizi wa sekta za huduma za kijamii, hasa afya, elimu, na maji, kwa kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika kwa ufanisi, miundombinu inakamilika kwa wakati, na huduma zinawafikia wananchi kama ilivyokusudiwa.

- Kuimarisha matumizi na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA kwa kuhakikisha muunganiko wa mifumo, kupunguza marudio ya majukumu, na kuongeza uaminifu wa takwimu za kifedha na kiutendaji.

- Kuimarisha mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

Zaidi ya hayo, ni muhimu kwa wadau wote ndani ya mfumo wa uwajibikaji kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia misingi ya uwazi, uwajibikaji, na uadilifu wa kitaasisi, ili kuboresha utendaji wa Serikali na kuongeza imani ya umma.

Upatikanaji wa ripoti kwa umma

Ripoti hizi zimewasilishwa rasmi Bungeni na sasa zinapatikana kwa umma. Zinaweza kupatikana kwa urahisi kupitia:

- Tovuti rasmi ya **NAOT (www.nao.go.tz)**

- Mitandao rasmi ya kijamii ya NAOT, ikiwemo **X (zamani Twitter), Facebook, na Instagram (@ukaguzitanzania)**

- Njia rasmi za mawasiliano za serikali zinazotumika kusambaza taarifa za ukaguzi kwa umma

Imetolewa na:

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.